TANESCO MTANDAONI

Toleo namba 23

Jarida la Mtandaoni | Juni 17, 2024




# **TANESCO** inavyotangaza utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma zake kwenye maonesho nchini

- Yahimiza wananchi juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ya umeme
- Yaeleza juhudi za utekelezaji wa miradi ya uzalishaji umeme kwa kutumia vyanzo mseto
- Maendeleo ya JNHPP kwa uhalisia pepe yawafurahisha wananchi kwa kasi ya utekelezaji wake
- Elimu ya usalama na kujiepusha na majanga ya moto yatolewa



# **TANESCO** Yashiriki Kilele cha Mkutano wa Uzinduzi wa **Nishati Safi** ya Kupikia **Barani Afrika** nchini **Ufaransa**

**Na. Adelina Lyakurwa, Ufaransa**

Mkurugenzi Mtendaji (TANESCO) Mha. Gissima Nyamo-Hanga tarehe 12 hadi 15 mei 2024 alialikwa kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Nishati Safi ya kupikia uliofanyika Nchini Ufaransa, ambapo Wakuu wa nchi mbalimbali duniani walihudhuria.

Katika Mkutano huo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa Mwenyekiti mwenza wa shughuli hiyo akishirikiana na Mheshimiwa Jonas Gahr Store Waziri Mkuu wa Norway, Ndugu Akinumwi Adenesia, Raisi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na Ndugu Fatih Birol Mkurugenzi Mtendaji "International Energy Agency".




Aidha Tanzania imeshirikishwa kwenye mkutano huo kutokana na jitihada kubwa zinazofanyika ndani ya nchi kusukuma ajenda hiyo ya kuwawezesha watu wote kutumia nishati safi ya kupikia ili kulinda afya za watu wao na mazingira.

Mkutano huo ulilenga kuifanya nishati safi ya kupikia iwe ajenda ya kimataifa na ipate wadau wengi zaidi, kuchukua hatua madhubuti za kisera zinazoweza kuharakisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Lengo lingine lilikuwa ni washiriki wa nchi zilizoendelea (Africa) na taasisi za fedha za kimataifa kutoa ahadi za fedha na msaada na nchi kutoa ahadi za kubadilisha sera na sheria ili kuharakisha matumizi ya nishati safi.

Ushiriki wa Mha. Gissima nchini Ufaransa ulitoa fursa ya kuzungumza na wafadhili / wahisani wa maendeleo na kufanya majadiliano juu ya ushirikiano na TANESCO katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia yanayoendelea nchini.

Majadiliano hayo bado yanaendelea ili kufikia muafaka jinsi ya kuungana katika kutekeleza adhma ya Serikali ya kufikia asilimia 80 kuwa na nishati safi ya kupikia kwa wananchi wake ifikapo mwaka 2034.

Kwa upande mwingine, lengo kuu la Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) chini ya Wizara ya Nishati kushiriki kikao hicho ni kuunga mkono Sera ya Serikali ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwemo umeme.

Pamoja na hayo TANESCO imeanza kufanya jitihada ya kuanza kuhamasisha wafanyakazi na wateja wake kutumia nishati safi ya kupikia.

Kuanzia mwezi Juni mwaka 2024 TANESCO kwa kishirikiana na kampuni ya nishati safi na endelevu TaTEDO-SESCO itazindua mradi wa kusambaza na kuuza majiko sanifu yanayotumia umeme (Efficient Electric Cooking Stoves) yapatayo 10,000 kwa wateja wa ndani na wa nje ya Shirika.







Mha. Gissima Nyamo-Hanga na aliyekuwa Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu Bi. Zuhura Yunus pamoja na viongozi wengine wa TANESCO walioshiriki kwenye mkutano huu



# **Serikali** Imejipanga Kuondoa Changamoto Ya **Umeme Tanzania**

**Ampongeza Rais Dkt. Samia kwa kutenga shilingi trilioni 8.18 sekta ya Nishati**

**Na. Charles Kombe, Dodoma**

Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alisema Serikali chini ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuondoa kabisa changamoto ya umeme nchini ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutekeleza miradi ya nishati ambapo katika kipindi cha miaka mitatu zaidi ya shilingi trilioni 8.18 zilitolewa.

> Maono na maelekezo yake kuhusu usimamizi wa sekta hii yamekuwa na mchango mkubwa katika ufanisi wa shughuli za sekta, katika hili, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka kipaumbele kikubwa katika utekelezaji wa miradi ya nishati
>
> **- Mhe. Kassim Majaliwa**

> Katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa umeme nchini, tayari nchi yetu imeanza kutumia umeme wa bwawa la Julius Nyerere Hydropower Project (JNHPP). Huu ni ushindi na kielelezo tosha kwamba Mama yupo kazini
>
> **- Mhe. Kassim Majaliwa**

Alitoa pongezi hizo Aprili 19, 2024 wakati akifunga Maonesho ya Wiki ya Nishati yaliyofanyika kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma.

Waziri Mkuu alipongeza TANESCO kwa kuweza kuzalisha umeme zaidi ya mahitaji yaliyopo sasa.

> Leo uzalishaji wa umeme ni mkubwa, Shirika letu la TANESCO limemudu kuzalisha umeme zaidi ya mahitaji tuliyonayo na Bwawa la Julius Nyerere Hydropower Project limeanza kazi na tayari megawati 235 ziko kwenye mfumo
>
> **- Mhe. Kassim Majaliwa**

Ameitaka Wizara hiyo iweke mkakati wa kuhakikisha maonesho hayo yanakuwa endelevu ili Waheshimiwa Wabunge waweze kupata fursa ya kuwasilisha hoja zao mahsusi na kutatua kero za wananchi wanaowawakilisha.

Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya washiriki wa maonesho hayo ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita, Waziri Mkuu alitaka Wizara hiyo ione uwezekano wa kuandaa maonesho kama hayo katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri. “Wakurugenzi wa Kanda na Mameneja wa Mikoa na Wilaya mko hapa. Nendeni mkae na muangalie jinsi ya kutekeleza jambo hilo,” alisisitiza.

Alitaka Wizara hiyo iweke mkakati wa kuhakikisha wananchi wote wanapata ufafanuzi wa masuala mbalimbali kuhusu fursa zinazopatikana kutokana na miradi inayotekelezwa na sekta ya nishati. “Pamoja na kuyaleta maonesho hapa Bungeni, kuna haja ya kupeleka maonesha kama haya kwenye maeneo ya katiati ya mji ili muweze kuwafikia wananchi wengi zaidi na kujibu hoja zao,” alisema.

Mapema, akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na wadau mbalimbali walioshiriki maonesho hayo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko aliipongeza TANESCO kwa kuendelea kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha wananchi wanapata nishati ya umeme.

Naye, Spika wa Bunge la Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson amesema sekta ya nishati ni kati ya sekta mtambuka kwa sababu inalisha sekta nyingine nyingi na ikitikisika, inatikisa na maeneo mengine pia.

Amesema pamoja na utoshelevu wa umeme kwenye gridi ya Taifa, ili kuwe na maendeleo bado nchi inahitaji umeme wa kutosha na hasa kwenye viwanda na siyo kuwasha taa za majumbani.

Naye, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mha. Felchesmi Mramba amesema ushiriki wa mwaka huu umevunja rekodi kwani watu zaidi ya 480 walitembelea maonesho hayo ambapo 267 walikuwa ni Waheshimiwa Wabunge.

Aliyataja maeneo ambayo washiriki walikuwa wakiuliza zaidi ni umeme, nishati ya jua, nishati jadidifu, nishati safi ya kupikia, mafuta na gesi.



# Matukio Katika Picha **Maonesho** Ya **Mazingira**




Waziri wa nchi ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Selemani Jafo akipata maelezo kutoka kwa Bw. Innocent Lupenza juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na TANESCO katika kulinda mazingira na miradi rafiki ya mazingira katika maonesho ya wiki ya mazingira viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dodoma




Naibu Mkurugenzi Mtendaji Usambazi Umeme TANESCO Mha. Nangali akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa TANESCO katika wiki ya mazingira iliyofanyika katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dodoma




# Si Majanga Yote ya **Moto** Majumbani Yanasababishwa na **Umeme** wa **TANESCO**

- **Matumizi ya wakandarasi wasio na utaalamu (Vishoka) kutandaza nyaya (wiring) pasipo kuwa na utaalaamu wa kufanya hivyo**
- **Matumizi holela ya vyombo mbalimbali vinavyohitaji kutumia nishati ya umeme visivyotengenezwa kwa ubora**
- **Matumizi Mabaya ya Nishati zingine vyatajwa kuongoza kama chanzo cha majanga ya moto nchini**

**Na Salama Kasamalu, Geita**

Kamanda wa Jeshi la zima moto na Uokoaji Mkoani Geita, Mrakibu Hamis Dawa, amesema kuwa si majanga yote ya moto yanayotokea majumbani huasababishwi na umeme unaotoka TANESCO bali matumizi holela ya vyombo vya Umeme pamoja na kutochukua tahadhari ya vifaa bora na Mkandarasi sahihi aliyehakikiwa kwa ajili ya kutandaza nyaya katika nyumba zao.

Kamanda Mkaribu aliyasema hayo Mei 24, 2024 alipotembelea Banda la TANESCO , katika maonesho ya Biashara ,Viwanda na Kilimo yaliyofanyika Mkoani Geita.

Alisema, mara nyingi inapotokea moto majumbani au viwandani cha kwanza wananchi ni kutupa lawama kwa umeme wa TANESCO kama chanzo cha moto huo, kabla ya kusubiri ripoti ya uchunguzi kutoka katika Jeshi hilo.




**Hamis Dawa Kamanda Mrakibu wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji Mkoani Geita**

Aidha, alisema kuwa jukumu la TANESCO ni kupeleka umeme kwa mteja mpaka kwenye mita lakini suala la umeme ndani ya nyumba ni suala la mteja kuhakikisha nyaya ndani ya nyumba yake zimetandazwa vizuri, na vifaa vyote vilivyotumika vina ubora ikiwemo kikata umeme (Circuit breaker).

Akizungumza juu ya matumizi holela ya vyombo vinavyohitaji nishati ya umeme yanayoweza kupelekea majanga ya moto, Kamanda Mrakibu alisema kwamba ni muhimu kwa watumiaji umeme kuhakikisha wanatumia vifaa vya umeme vyenye ubora kwa umakini na kuzima kila baada ya kutumia vifaa hivyo.

> Kuna vifaa vingine vya umeme vinaweza kujizima vyenyewe baada ya kutumia umeme kwa kiwango kinachotakiwa (energy efficiency) na vina uwezo wa kudhibiti umeme. Vifaa hivyo ni kama AC na jokofu, lakini vifaa kama pasi na jiko, unaposahau kuzima baada ya matumizi vinaweza kuwa chanzo cha moto, na utasema tatizo ni umeme wa TANESCO lakini chanzo ni matumizi holela yasiyozingatia utaratibu sahihi wa kuvitumia
>
> **- Kamanda Hamis Dawa**


Aliongeza kwa kusema kuwa, katika matumizi ya Nishati safi ya kupikia Jeshi la Zimamato na uokoaji limeanza kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya Nishati safi ya kupikia ikiwa ni Nishati ya umeme na gesi ili kuepusha majanga ya moto.

Kwa upande wake Meneja wa TANESCO Mkoa wa Geita, Mha. Joachim Ruweta, alisema kuwa TANESCO Mkoa wa Geita inashirikiana kwa ukaribu na Jeshi la zima moto na Uokoaji Mkoani humo kwa kufanya kazi kwa kushirikiana kwani kazi zao zinategemeana.

> Tunafanya kazi kwa ushirikiano sana na Jeshi la zima moto hapa Mkoani Geita, wanapopokea taarifa ya moto, wanatupigia na sisi ili twende kuzima umeme, kwa sababu kuna kemikali zingine wanazozitumia, haziendani na umeme, hivyo wao hawawezi kuzima moto bila kutushirikisha
>
> **- Mha. Joachim**



Akihitimisha Mha. Joachim alitoa rai kwa wananchi kutumia vifaa vya umeme kwa umakini na kukagua njia za umeme ndani ya nyumba zao kila baada ya Miaka 5, ili kuepuka matatizo mbalimbali ya umeme kama upotevu wa umeme na majanga ya moto.



Mwananchi wa **Geita** akipata huduma kutoka kwa afisa wa **TANESCO** kwenye **Maonesho ya Biashara** mkoani **Geita**




# **TANESCO** Mkoa wa **Geita** Yawahimiza Wawekezaji Kutumia Fursa Zilizopo Kuwekeza Kwani **Umeme** Upo wa Kutosha

**Na. Salama Kasamalu, Geita**

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Geita, Mha. Joachin Rweta aliwahimiza wakazi wa Mkoa wa Geita na Mikoa ya jirani kutumia fursa ya umeme Mkoani Geita katika kufanya Uwekezaji kwani hali ya umeme katika Mkoa wa Geita ni nzuri.

Mha. Joachim aliyasema hayo Mei 27, 2024 katika maonesho ya Biashara, viwanda na Kilimo, yaliyofanyika katika viwanja vya EPZA, Bomba mbili, Mkoani Geita. Aliesema kuwa, dhima kubwa ya TANESCO kushiriki maonesho haya ni kutangaza fursa ya uwekezaji kwa wafanyabiashara na watu wa viwanda kufanya uwekezaji ndani ya Mkoa wa Geita ikiwa ni mkakati mmoja wapo wa Shirika kujiendesha kibiashara.

> Niwahakikishie wakazi wa Geita na Mikoa ya jirani kuwa umeme upo wa kutosha, hivyo msiogope kuja kuwekeza kwenye ukulima kufungua mashine, uwekezaji wa viwanda, na biashara mbalimbali zinazotumia umeme
>
> **- Mha. Joachim**

Sambamba na hilo, Mha. Joachim amewataka wafanyabiashara wa vifaa vya umeme hasa majiko ya kupikia, kufanya biashara hiyo katika Mkoa wa Geita ili iwe fursa kwa wananchi wa Geita kuweza kutumia nishati ya umeme Kama nishati safi ya kupikia.

> Wafanyabiashara iwe fursa kwenu kuwekeza kwenye biashara ya vifaa vya umeme hapa Geita, na hasa majiko ili wananchi wa Geita waweze kutumia Nishati hii safi kwa kupikia
>
> **- Mha. Joachim**

Mmoja wa mteja aliyetembelea katika banda la TANESCO katika maonesho hayo, Mha. Zepheline Biseko alisema kuwa amefurahishwa na huduma nzuri aliyoipata, ikiwemo elimu ya kutosha ya matumizi bora ya umeme na miradi mbalimbali ya uwekezaji katika sekta ya Nishati nchini.

Aliongeza kwa kusema kuwa uwepo wa umeme wa kutosha Mkoani Geita, umemsaidia katika shughuli zake za ujenzi wa majengo ya kisasa hasa katika kutumia mashine za upasuaji mawe na kuchomelea.



**Afisa wa TANESCO, Lucas Swere akizungumza na wananchi mbalimbali waliojitokeza kwenye maonesho hayo.**




# TANESCO Yaifikisha JNHPP Kwenye Maonesho Ya Biashara Mbeya

**Na. Shamu Lameck, Mbeya**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilishiriki maonesho ya biashara Mbeya katika kuonesha mchango wake kwenye kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa maonesho hayo tarehe 24, Mei, 2024 Mkuu wa Mkoa Mbeya Mhe. Juma Zuberi Homela aliipongeza taasisi na kampuni zote kwa ushiriki wao kwenye maonesho hayo.

Alisema kuwa maonesho hayo yanatoa fursa ya kuonesha wananchi huduma ambazo kila taasisi inatoa na mikakati yake katika kuendelea kuboresha huduma hizo.



> Tunapozindua maonesho haya ya pili ya biashara hapa Mbeya, niwapongeze wote kwa kuja kuonesha huduma na bidhaa zenu, hii ni sehemu nzuri kwa wananchi kuja kujifunza na kujionea shughuli zenu,
>
> **- Homela.**

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA) ndugu Erick Schinga alieleza kuwa, wakati wa siku za maonesho walitarajia ugeni wa mabalozi kutoka Namibia, Malawi, na Zimbabwe kuja kutembelea maonesho hayo.

TANESCO katika maonesho hayo imeshiriki kuonesha namna ambavyo wamejipanga kuendelea kuchangia shughuli za uwekezaji nchini kwa kuonesha miradi ya kimkakati ya uzalishaji umeme ikiwemo mradi wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP), mradi umeme jua Kishapu - Shinyanga na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya umeme nchini.



Rais wa TCCIA Erick Schinga akipata elimu na maelezo kwenye banda la TANESCO kwenye maonesho ya biashara ya Mbeya City Expo



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya Mhe. Beno Malisa akikabidhi cheti cha ushiriki wa maonesho ya biashara Mbeya City expo kwa Shirika la umeme Tanzania (TANESCO)





Wananchi wakitazama mradi wa JNHPP kwa kutumia teknolojia ya uhalisia pepe kwenye maonesho ya biashara mkoani Mbeya



# **TANESCO** Yaelimisha Wananchi Juu ya Umuhimu wa Matumizi Ya **Nishati Safi** ya Kupikia ya **Umeme**

**Na. Leopodina Kushoka, Tanga**

TANESCO ilitoa elimu kwa wananchi waliotembelea Banda la TANESCO katika maonesho ya biashara na Utalii yaliyofanyika katika viwanja vya Usagara, Mkoani Tanga.

Akizungumza katika Maonesho hayo, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tanga Mha. Mathias Solongo amesema kuwa Moja wapo ya elimu inayotolewa katika Banda la TANESCO ni juu ya umuhimu wa kutumia Nishati safi ya umeme kupikia, ambapo aliwataka wananchi kutumia Majiko ya umeme na kuachana na matumizi ya Kuni kwani matumizi ya Kuni hupelekea athari kwa watumiaji na uharibifu wa mazingira.

> Hapa tunatoa elimu ya matumizi bora ya umeme, ikiwemo matumizi ya umeme kwenye kupikia kama Nishati safi, kuna majiko mbalimbali yapo hapa na vifaa vyake hivi vyote tumevileta hapa kama mfano tu wa namna gani unaweza kutumia nishati safi ya umeme kupikia, bila kutumia umeme mwingi na hivyo kupunguza gharama
>
> **- Mha. Solongo**

Sambamba na hilo Mha. Solongo aliwashauri wateja wa TANESCO na wananchi kwa ujumla ambao wanataka kujiunga na huduma ya umeme kutumia mfumo wa Nikonekt.

> Sasa huduma zetu zinapatikana kiganjani kwako kupitia simu yako ya mkononi, huna haja ya kuja mpaka TANESCO, huduma zetu zipo karibu na wewe na kama una changamoto juu ya matumizi ya Nikonekt karibu sana kwenye banda letu tutakuelekeza namna ya kutumia huduma hii
>
> **- Mha. Solongo**

Naye Mkazi wa Mkwakwani Bi. Mariam Mbwana ambaye ametembelea banda la TANESCO katika maonesho hayo alisema kuwa amepata elimu aliyopata imemsaidia na kuwa ataanza kutumia umeme kama nishati safi ya kupikia kwani amekua akitumia gharama kubwa katika matumizi ya mkaa.

TANESCO ni moja ya taasisi zilizoshiriki maonesho hayo Mkoani Tanga, dhumuni kubwa ikiwa ni kuwa fikia wateja na kujua changamoto zao sambamba na kutangaza Miradi ya kimkakati katika sekta ya Nishati inayotekelezwa na Serikali.

# Matukio Katika **Picha** Maonesho ya **Biashara Tanga**



Wanafunzi wakitazama mradi wa JNHPP walipotembelea banda la TANESCO kwenye Maonesho ya Biashara Tanga




Wananchi wakielimishwa juu ya matumizi sahihi ya Nishati safi ya kupikia walipotembelea banda la TANESCO



Wananchi wakipewa elimu sahihi juu ya Nishati safi ya kupikia kwenye maonesho ya biashara Tanga



# **TANESCO** Yatakiwa Kuhimiza Matumizi Ya **Nishati Safi** Ya **Kupikia**

**Na. Amanda Mokami Tagame, Dar es salaam**

TANESCO iliagizwa kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuwa mstari wa mbele katika kutekeleza hayo kwani ni maono yanayosimamiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

Hayo yameelezwa na Mha. Innocent Luoga Kamishna wa umeme na nishati jadidifu wakati alipotembelea banda la TANESCO katika maonesho ya wiki ya nishati jadidifu yaliyoanza tarehe 6 Juni, 2024 jijini Dar es Salaam.

> Kuweni mstari wa mbele kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia ya umeme kwa wananchi kama Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan anavyoibeba ajenda hii na kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wanawake barani Afrika
>
> **- Mha. Luoga**

Pia, aliwasihi kuhakikisha kuwa wanatumia vyanzo mseto vya kuzalisha umeme na kutumia nishati jadidifu ikiwemo umeme jua, jotoardhi ili kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika.



> TANESCO mjikite kwenye kuongeza uwekezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu ili tuweze kuwa na uhakika wa kuwa na vyanzo vya kutosha vitakavyotupa umeme wa uhakika nchini
>
> **- Mha. Luoga**

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa TANESCO Bi. Irene Gowelle alieeleza kuwa, TANESCO inaendelea kuhimiza juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ya umeme kwani umeme ni nishati safi, rafiki wa mazingira na gharama nafuu.

> Mhe. Rais. Dkt. Samia amekuwa mstari wa mbele katika kusisitiza juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Sisi kama Shirika tuko mstari wa mbele katika kumuunga mkono kwa kuwapa elimu wateja juu ya umeme kama nishati safi ya kupikia na ya gharama nafuu
>
> **-Bi. Gowelle**

TANESCO ilishiriki maonesho ya wiki ya nishati jadidifu yaliyofanyika kwa siku mbili Dar es salaam kuanzia tarehe 6 Juni, 2024 yaliyokuwa na lengo la kukutanisha wadau mbalimbali wa nishati jadidifu.




Mha. Innocent Luoga akitoa maelekezo kwa TANESCO alipotembelea banda hilo katika wiki ya nishati jadidifu akiwahimiza juu ya umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kama kipaumbele cha Serikali ya awamu ya sita.




Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa umma Bi Irene Gowelle akizungumza na waandishi wa habari katika ufunguzi wa maonesho ya Wiki ya Nishati jadidifu yaliyofanyika jijini Dar es salaam



Wataalam kutoka TANESCO wakimpatia maelezo mgeni rasmi katika maonesho ya wiki ya nishati Mha. Innocent Luoga alipotembelea banda la Shirika hilo




Makamu wa Rais Mhe. Philip Mpango akipokea maelezo kutoka kwa Mha. Rose Lutenganya wakati alipotembelea banda la TANESCO katika maonesho ya FIDIC



**Wahandisi kutoka TANESCO wakifurahia kuona maendeleo ya JNHPP kupitia uhalisia pepe**



**Mmoja wa washiriki wa kongamano la wakandarasi (FIDIC) akitazama maendeleo ya mradi wa Julius Nyerere kupitia teknolojia ya uhalisia pepe**




# TANESCO Mara Yashiriki Maadhimisho Ya Kimataifa Kupinga Ukatili Dhidi Ya Wazee.

**Na. Joyce Makori, Bunda Mara**

Maadhimisho ya kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya wazee yameazimishwa wilayani Bunda Mkoa wa Mara tarehe 15 Juni, 2024.

Katika maadhimisho hayo elimu na taarifa mbalimbali zinazohusu Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO ) zilitolewa kwa wananchi pamoja na wateja ikiwemo, Mabadiliko ya mfumo wa LUKU yanayoendelea hivi sasa, Elimu kuhusu UMETA, Elimu ya JISOTI na taarifa mbalimbali za mafanikio ya Shirika katika utekelezaji wa miradi ya umeme ya kimkakati pamoja na miradi ya vitongoji inayoendelea na miradi ya ujazilishi.

Katika kutoa elimu wakati wa kutembelea mabanda, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Mara Mha. Nickson Babu aliweza kuelezea kwa mgeni rasmi Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mara Kanal Evans Mtambi juu ya umuhimu wa ushiriki wa TANESCO kwenye maonesho hayo ikiwa ni pamoja na jitahidi za Shirika kuhakikisha wazee wetu ambao ni tunu ya Taifa wanapata huduma ya Umeme lakini vile vile si kupata huduma ya umeme tu bali umeme wa gharama nafuu.

Mhandisi Babu alisema kuwa, lengo la TANESCO kubuni kifaa cha UMETA ni kumuwezesha Mteja ambaye hana uwezo wa kusuka nyaya za umeme kwenye nyumba yake kuweza kupata huduma ya umeme kwani changamoto kubwa imeonekana ni gharama za kusuka waya (Wiring) kuwa kubwa kiasi cha kumshinda mteja na hasa wazee wetu ambao umri wao umekwenda na uwezo wa vipato vyao kuwa mdogo kutokana na kushindwa kabisa kujishughulisha na shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato.

Sambamba na hilo, tumeweza kutoa huduma ya umeme bure kwa wazee wawili Wilayani Bunda Kijiji cha Kiloleli mmoja wao akiwa ni Mzee James Gidioni mwenye umri wa miaka 82 ambaye ameishukuru sana TANESCO kwa kuweza kumuangazia maisha katika umri wake huo kwani tangia kuzaliwa kwake hajawahi kutumia huduma hiyo.

> Nipende kuwashukuru watu wa TANESCO na Serekali yetu kwa kuweza kuniletea huduma hii ya umeme kwani itanifanya kuongeza siku zangu za kuishi kwa furaha niliyoipata leo
>
> **- Bw. James.**

Vile vile changamoto mbalimbali za Wateja zilizowasilishwa katika maonesho hayo ziliweza kutatuliwa ikiwa ni pamoja na kufika kwenye makazi ya wateja kushuhudia na kutoa suluhisho hapo hapo.

# Matukio Katika **Picha** Maadhimisho Ya Kimataifa Kupinga Ukatili Dhidi Ya Wazee




Mkuu wa Mkoa wa Mara Mhe.  Kanali Evans Mtambi akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa TANESCO mkoa wa Mara Mha.Nickson Babu juu ya huduma zetu wakati wa maadhimisho ya kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya wazee.




Mhandisi Nickson Babu ( Wa kwanza kulia)  akitoa elimu kuhusu kifaa cha UMETA kwa Mkuu wa Mkoa wa Mara na kuelezea umuhimu wa kifaa hicho.

# Matukio Katika **Picha** Maadhimisho Ya Kimataifa Kupinga Ukatili Dhidi Ya Wazee




Mzee James Gidioni akitoa shukurani na kuelezea furaha yake kwa Shirika la Umeme Tanzania ( TANESCO ) mkoa wa Mara baada ya kuunganishiwa huduma ya umeme bure wakati wa maadhimisho ya kimataifa ya kupinga ukatili dhidi ya wazee



# Ujumbe wa MD



Ndugu Wafanyakazi,

Kama mnavyofahamu, Shirika limekuwa likitekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa mfumo mkubwa wa TEHAMA ambao unatambulika kama Duma. Ninayo furaha kuwashirikisha taarifa za maendeleo yetu katika safari hii ambayo tulianza takribani miaka 10 iliyopita. Nina furaha kuona ndoto hii ikitimia. Hii ni hatua muhimu sana kwa shirika letu tunapoendelea kutekeleza mkakati wetu wa miaka 10.

Kidijitali imebainishwa kuwa moja ya mwelekeo mkubwa wa kimataifa unaolenga kuleta mabadiliko makubwa ya taasisi zinazotoa huduma za umeme. Ili kufikia Dira yetu "Kuwa mtoaji bora wa suluhisho za nishati zinazochochea ustawi endelevu wa kiuchumi Afrika," ni muhimu Shirika kuwezesha mipango ya kidijitali kwa ujumla.

Duma ina jukumu la kimkakati katika kuwezesha ufikiaji wa malengo yetu ya muda mrefu, kuleta thamani kwa wateja wetu wa ndani na nje, kurahisisha utendaji, na kuongeza ufanisi. Mimi binafsi kwa kushirikiana na Timu ya Uongozi wa Shirikatunatambua na kuunga mkono kikamilifu mradi wa Duma, tukitambua umuhimu wake katika kuyafikia manufaa makubwa ya Shirika letu.

Natoa wito kwa viongozi na wafanyakazi wote kuunga mkono, kushiriki, kukubali na kusukuma mbele utekelezaji wa mfumo wa Duma kwa manufaa ya jumla ya shirika letu.

Ninatambua na kuthamini kujitolea kwenu na jitihada zenu katika kusukuma mradi huu hadi ukamilike ili tuweze kupata faida zake kikamilifu. Pamoja, tuendelee kufanya kazi kufikia mustakabali mzuri wa shirika letu.

Kwa hakika, tupo kwenye uelekeo sahihi wa kuwa Fasta Pamoja!

Wenu katika kujenga TANESCO yenye Ufaninsi,

Mha. Gissima Nyamo-Hanga
Mkurugenzi Mtendaji, TANESCO

## Bodi Ya **Wahariri**

1. Mha. Gissima Nyamo-Hanga - Mwenyekiti
2. Irene Gowelle - Mhariri Mkuu
3. Amanda Tagame - Mhariri
4. Salama Kasamalu - Mwandishi
5. Shamu Lameck - Mwandishi
6. Leopodina Kushoka - Mwandishi
7. Adelina Lyakurwa - Mwandishi
8. Joyce Makori - Mwandishi
9. Charles Kombe - Mpiga Picha
10. Thomas Tito - Mpiga Picha
11. Michael Sokotta - Mbunifu Kurasa





TUFUATILIE KUPITIA

**KURASA ZETU ZA MITANDAO YA KIJAMII KUPATA TAARIFA SAHIHI ZA SHIRIKA**

www.tanesco.co.tz